56 Dk. A. C. Dixon anasema katika makala katika *London Christian* (16 Novemba 1911): “Angalieni ustaarabu huu ambao Mungu mwenyewe aliuanzisha, nanyi mtamsikia akisema: ‘*Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja*’. Mwanamke anapewa nafasi ya kwanza. Si mwanamke anayemwacha baba na mama na kuambatana na mumewe; bali ni mwanamume anayemwacha mama yake na baba yake na kuambatana na mkewe.” Katika jambo moja sikubaliani na Dk. Dixon. Ustaarabu uliojengwa juu ya sheria hii ya Mungu ya ndoa haukumfanya mwanamke kuwa bora kuliko mumewe, lakini ulimzuia asiwe chini yake. Katika jambo hili, habari ya Yakobo na wake zake, Lea na Raheli, inatufundisha. Anapotaka kuondoka kwa baba mkwe wake, anawaomba wake zake kwa upole waandamane naye. Wao hawasemi: “Ni wajibu wetu kumfuata mume wetu”, bali “Tuna sababu mbili za kwenda: Baba yetu hakutupa urithi; naye amejiwekea mshahara wa Yakobo, nao ulipaswa kulipwa kwetu na kwa watoto wetu” (Mwanzo 31:14-16). Kutokana na hili inaonekana kwamba huko walikoishi wanawake hawa, wanaume hawakuwauza binti zao katika ndoa, na kwamba wanawake hawakujiona kuwa wamefungwa na ndoa kuwafuata waume zao hadi mwisho wa dunia. Wataalamu wa lugha wanaotambuliwa wanasema kwamba Ibrahimu alimwambia Abimeleki (Mwanzo 20:13) kuhusu Sara: “*Kwa maana Mungu alimfanya atangetange pamoja nami*”, si tu “*Mungu aliponifanya ... nitangetange*”. Tofauti ya maana ni hii: Wakati huo haikutarajiwa kwamba mke angemfuata mumewe katika safari zake za kutangatanga, bali kinyume chake. Mungu alitaka Sara na Ibrahimu wote wawili watoke katika mazingira ya ibada ya sanamu; kwa hiyo anampa Sara ufunuo wa mapenzi yake, ili asifuate desturi ya kawaida ya kubaki kwa jamaa zake.

“Ustaarabu uliojengwa juu ya sheria hii ya Mungu ya ndoa haukumfanya mwanamke kuwa bora kuliko mumewe, lakini ulimzuia asiwe chini yake.”

Somo la 8 – HESHIMA YA MWANAMKE NYAKATI ZA AWALI

57 Profesa wa Cambridge Robertson Smith anaandika: “Kwa mujibu wa Mwanzo, ndoa inamaanisha kwamba mwanamume anamwacha baba yake na mama yake na kumgeukia mke wake, nao watakuwa mwili mmoja. Hilo linapatana kabisa na kile tunachokipata katika sehemu nyingine za historia ya mababu. Bw. McLennan amezitaja ndoa za Yakobo, ambapo Labani kwa wazi alikuwa na sheria upande wake aliposema kwamba Yakobo hakuwa na haki ya kuwachukua wake zake na watoto wao; na vilevile ukweli kwamba, Ibrahimu alipotafuta ‘mke kwa ajili ya Isaka’, mtumishi wake alidhani kwamba huenda sharti lingekuwa kwamba Isaka aje akae kati ya watu wa mwanamke huyo”. [Katika hali hii Ibrahimu hakuweza kukubali, kwa sababu Mungu alikuwa amemwita waziwazi aondoke katika ibada yao ya sanamu]. “Watoto wa Yusufu kwa mke wake Mmisri walikuwa Waisraeli kwa kuasiliwa tu; vivyo hivyo mke wa Samsoni kutoka kwa Wafilisti anabaki kwa watu wake, naye anamtembelea huko. Mambo haya yote yanaonyesha kile kinachoelezwa katika Mwanzo 2:24 kama aina ya asili ya ndoa.” Nasi tungeweza kuuliza, maneno haya ya zamani kabisa yanamaanisha nini, – “ataambatana na mkewe; nao watakuwa mwili mmoja”, kama si kwamba atakuwa wa nasaba ileile ya mke wake? Mwandishi huyo huyo anaandika: “Nasaba ya mama ndiyo aina ya asili ya ukoo, na umama wa pamoja ndio aina ya asili ya umoja wa kindugu, inayotawala lugha yote ya Kisemiti.” J. P. Peters, D.D., anaandika kuhusu kifungu hicho hicho cha Mwanzo: “Katika namna uhusiano wa mwanamume na mwanamke unavyoelezwa hapa, inaonekana tuna ushahidi mwingine wa kupita tu wa ukale mkubwa wa habari hii. Si mwanamke anayemwacha baba na mama na kuambatana na mwanamume, bali mwanamume anayemwacha baba na mama na kuambatana na mke wake. Inaonekana kana kwamba hapa tuna mabaki ya mfumo jike wa zamani, ule uhusiano wa ndoa ambao tuna mfano wake katika habari ya Samsoni, ambapo mke anabaki katika kabila lake, ukoo wake au familia yake, na anatembelewa na mume. Katika hali kama hiyo uzao ni wa familia ya mke, si wa mume” (*Early Hebrew Story*, uk. 223).

58 Mtaalamu mkubwa wa akiolojia, Prof. Flinders Petrie, pia ameandika mambo ya kuvutia juu ya jambo hili, nami ninatoa nukuu ndefu kutoka kwake, ili kuonyesha kwamba katika jambo hili sitii chumvi. Anaandika: “Tumezoea sana wazo kwamba wanawake wa Mashariki daima walikuwa tegemezi – kama walivyo sasa chini ya Umuhamadi –, hivi kwamba tunapaswa kufumbua macho yetu ili tuone mfumo tofauti kabisa unaoonyeshwa kwetu katika historia ya awali ya enzi ya mababu. Kwa jumla inaweza kusemwa kwamba mfumo wetu wa sasa, kwa upande mmoja, ni mchanganyiko kamili wa wanaume na wanawake katika jamii, na kwa upande mwingine wanaume wanabaki na haki zote na mali. Kanuni ya zamani ya Mashariki iliweka ulimwengu tofauti kwa wanaume na kwa wanawake, huku wanawake wakibaki na haki zao wenyewe na mali yao yote.”

“Nasaba ya mama ndiyo aina ya asili ya ukoo, na umama wa pamoja ndio aina ya asili ya umoja wa kindugu.”

59 Prof. Petrie anaendelea: “Mwanamke wa kwanza [mbali na Hawa] anayejitokeza katika AK¹ kama mtu mwenye haiba yake ni Sara, ‘mkuu wa ukoo’, kama jina lake linavyoonyesha. Sar ni jina la kawaida la zamani la chifu, ambalo bado linatumika katika Mashariki ya Kati. ... Hadhi yake ya kujitegemea inaonekana wazi kwa kuwa, bila kumtegemea Ibrahimu hata kidogo, aliishi katika jumba la Farao au katika baraza la Abimeleki. Hakuna jaribio la waandishi wa baadaye la kulieleza jambo hili kwa namna nyingine linaloweza kueleza uhuru huu, ambao katika miaka ya karibuni umepuuzwa tu.

“Sara alikuwa na makao yake ya kujitegemea huko Mamre, akaishi huko, wakati Ibrahim aliishi Beer-sheba; na inasemwa kwamba alikuja kumwombolezea na kumzika. Kwa hiyo hadhi yake wakati wa safari zake na katika maisha ya baadaye haikuwa hata kidogo ile ya utegemezi wa kufichwa nyumbani, bali ile ya mkuu wa ukoo anayejitegemea, au ‘mama wa kabila’.

60 “Kwa kuwa Sara hakuwa na binti, ilikuwa lazima kumleta mtu kutoka katika familia ili aongoze ukoo, na Rebeka akaletwa kutoka nchi ya zamani ya nyumbani. Hema la heshima la Sara lilihamishwa na Isaka, mwendo wa siku tatu au nne, kutoka Mamre hadi Beer-lahai-roi, na mara Rebeka alipofika, aliwekwa katika hema hilo. Baada ya hapo Isaka akamwoa; naye anaonekana kuwa alijitegemea vilevile kama Sara. Kwa kuwa Rebeka hakuwa na binti wa kumrithi, Yakobo ilimbidi amwoe Lea, aliyekuwa mkubwa katika mfuatano, wala hakuweza kumpata Raheli kabla nafasi ya Lea haijalindwa hivyo.

61 “Kabla ya kuhamia Misri ni binti mmoja tu anayetajwa kati ya wana kumi na mmoja, yaani Dina, ‘mwamuzi wa kike’ [kama maana ya jina hilo ilivyo], binti wa mkuu wa ukoo Lea. Ndugu zake walikasirika kuhusu kuolewa kwake na Mhivi², kwa sababu kwa njia hiyo angeweka cheo chake cha mwamuzi chini ya taifa lingine; na ni kuingizwa tu kwa Wahivi katika taifa la Israeli kwa njia ya tohara kulikoweza kuitengeneza hali hiyo (Mwanzo 34:1-24). Hata baadaye tunaweza kufuatilia nasaba hii katika jina la mwanamke pekee ambaye jina lake limetajwa kutoka kizazi kilichofuata: Sera (Mwanzo 46:17), umbo moja la jina Sara, ‘kiongozi wa kabila’. Kwa kuwa Dina inaonekana hakuwa na watoto, ilikuwa jambo la kawaida kumchukua mzao wa Zilpa, mjakazi wa Lea. Hivyo Asheri, ambaye Lea alifurahi sana juu yake, alitoa mkuu wa ukoo aliyefuata katika binti yake Sera.”

62 Sehemu fulani ya heshima hii ya awali ya mwanamke inaweza kufuatiliwa katika historia yote ya Biblia, hasa katika “mama wa mfalme”, aliyetumia mamlaka kando ya mfalme, ambaye anatajwa hata mwaka 600 KK nyakati za Yeremia, katika Yeremia 13:18 (hapa neno hilo mara nyingi linatafsiriwa vibaya kuwa “malkia”).

Kabla ya Kiebrania kulikuwa na lugha za Kiakadi na Kisumeri; na Prof. Sayce anasimulia kwamba watafsiri wa nyimbo za zamani za Kisumeri katika lugha ya Kisemiti walibadilisha “kike na kiume” kuwa “kiume na kike”, na kuingiza mabadiliko mengine ya namna hiyo ili kuwapa wanaume ukuu. Sumeri, Akadi, Babeli, Arabia, Foinike na Misri – ustaarabu huu wote wa zamani kabisa ulitambulishwa na sifa za mfumo jike. Sir Wm. Ramsay anasema vivyo hivyo kuhusu Asia Ndogo. Nasaba ya kike inaweza pia kuthibitishwa katika Ugiriki ya zamani – mwanamke wa Sparta alikuwa wa mwisho kupoteza heshima yake. Hata karibu mwaka 450 KK Herodoto aliandika kuhusu Walikia: “Mtu akimwuliza jirani yake yeye ni nani, atasema kwamba alizaliwa na mama fulani, na atawataja mababu wa mama yake.” Zamani ilidhaniwa kwamba sababu ya jambo hili ilikuwa kwamba baba alikuwa na zaidi ya mke mmoja; lakini leo inasisitizwa kwa nguvu kwamba hiyo si maelezo sahihi. Hata neno la Kigiriki la “ndugu” (*adelphos*) linaeleza undugu kupitia mama, si kupitia baba.

63 Tumeiacha sheria ya Mungu mbali sana hivi kwamba leo, kwa mujibu wa sheria ya Uingereza, mama si mzazi. Wakati wa utawala wa Edward VI, mahakama za kiraia na za kanisa kwa pamoja zilitangaza kwamba Duchess wa Suffolk hakuwa ndugu wa mwana aliyemzaa. Kanisa la Uingereza linapinga talaka kwa ukali. Lakini tukisoma katika Mathayo 19 agizo la Bwana Yesu kuhusu talaka, tunagundua kwamba hitimisho, “*Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe*”, limejengwa juu ya msingi huu: “*Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja*”. Kanisa halitaweza kamwe kutekeleza kwa ufanisi hitimisho la agizo hili [marufuku ya talaka, maelezo ya mtafsiri] maadamu linapuza misingi ambayo agizo hilo limejengwa juu yake.

64 Sarufi zetu za Kiebrania na kamusi zinaonyesha kwamba karibu majina yote ya jumla yanayohusu mataifa, na majina ya miji na jumuiya, ni ya *jinsia ya kike*. Ilikujaje hivyo, hasa kwa kuwa haiwezekani kabisa kufikiri kwamba wanaume nyakati za Kristo walibuni neno la jinsia ya kike ili kueleza umati wa watu kama ule ambao Kristo aliulisha? Kwa mujibu wa habari ya Injili aliwalisha *“wanaume elfu nne, bila wanawake na watoto”*. Na wakati mwingine aliwalisha *“wanaume elfu tano, bila wanawake na watoto”*. Tena, katika Matendo ya Mitume Petro, Stefano na Paulo wanaihutubia mikutano ya watu katika nyakati mbalimbali kama *“Waume, ndugu”* wala hawawataji wanawake hata kidogo. Mwanamume anapochukua nafasi ya kwanza karibu peke yake, katika umati ni jinsia yake tu inayotajwa. Hata hivyo inaeleweka vizuri kwamba katika nyakati ambapo ukoo wa damu ulihesabiwa kupitia wanawake, taifa au jumuiya ya damu moja ilipotajwa, mataifa, miji, jumuiya na mikutano ya watu yalipewa majina ya kike. Majina haya ya jumla ya miji, vijiji n.k. yalikuwa ya kike kwa sababu mahali hapo palikuwa na *vikundi vya nyumba zilizomilikiwa na wanawake*, ambazo wanawake hao hawakuhamu kutoka humo mara nyingi. Neno la miji katika Hesabu 21:25, Yoshua 15:45 n.k. ni *“binti”*. Kwa sababu hiyo hiyo katika Isaya 12:6, badala ya *“wakazi wa Sayuni”*, maandishi ya asili yanasema *“mkazi wa kike wa Sayuni”*, na mifano kama hiyo ni mingi sana katika AK.

Somo la 9 – UCHAGUZI WA HAWA NA UCHAGUZI WA ADAMU

65 Katika mfululizo wa mihadhara yenye msaada kuhusu *“Uhakiki wa Kiroho wa Biblia”*, Dk. A. T. Pierson alisema: *“Katika ulimwengu wa akili mtu anaamini jambo kwa sababu ni kweli; katika ulimwengu wa roho mtu anajua kwamba jambo ni kweli kwa sababu analiamini.”* Ikiwa mnaye Roho pamoja nanyi ili awathibitishie ukweli, na ikiwa mnaamini yale yanayosemwa leo katika somo letu, basi *upokeeni ukweli*, ishini kwa kuufuata na wafundisheni wengine, hata kama unaweza kugeuza kabisa mafundisho mliyopokea hapo awali na chuki mlizoweza kuzichukua.

66 Katika muktadha wa masomo haya, na tuikatae mara moja kwa daima kila tamaa ya kutaka kujua *“nani aliye mkubwa katika ufalme wa mbinguni, mwanamume au mwanamke”*, kama swali lisilostahili. Lakini kama wanawake, tunajali hatima ya mwanamke, na tunapaswa kuijali. Hatima hii iliwekwa katika bustani ya Edeni. Ni ipi?

67 Tafadhali someni Mwanzo 2:17-18. Muda mfupi kabla ya kutenganishwa kwa jinsia, Adamu alipokuwa amefikia ukomavu wa kuwajibika na alipaswa kutoa hesabu ya mwenendo wake, Mungu alimkataza kula matunda ya *“mti wa ujuzi wa mema na mabaya”*. Hawa alikuwa bado *“hajafanyizwa”*, kama mstari wa 18 unavyoonyesha; amri ilitolewa katika nafsi ya pili umoja. Hatuambiwi *“mti”* huo ulikuwa nini hasa. Inaruhusiwa kufikiri kwamba neno *“mema na mabaya”* kwa vitendo lina maana sawa na *“maumivu na anasa”*, kama linavyotokea katika vifungu kama 2 Samweli 19:35, Ayubu 2:10, Isaya 7:15-16, Yereimia 42:6 n.k. Matokeo ya Adamu kutotii sheria kama hiyo yangukuwa, kwanza, kugundua tofauti iliyo wazi kati ya *“maumivu”* na *“anasa”*, na pili, kishawishi kikubwa cha kutafuta anasa siku zijazo na kuepuka kila *“maumivu”*, hata yale yenye manufaa. Labda Mungu alitaka kuelekeza fikira za Adamu kwenye nia na kanuni za mwenendo zilizo juu zaidi kuliko *“maumivu na anasa”* tu. Katazo hili, tukilieleza hivyo, lilikuwa na umuhimu wa pekee, kwa kuwa lilitangulia moja kwa moja tukio la Mungu kumpa Adamu mke. Zaidi ya yote, kuyakwepa maumivu ya kuwajibika katika uhusiano wa jinsia mbili ni jambo la kukataliwa. Kunamaanisha kuharibika kwa mtu binafsi na hatimaye kuharibika kwa jamii ya wanadamu; na lazima kulete mateso na mzigo kupita kiasi upande wa jinsia ya akina mama.

68 Hawa “alifanyizwa” baada ya katazo hili kuwa limekwisha kutamkwa, wala hatuambiwi kama baadaye alilisikia kutoka kwa Mwenyezi, au kama alilijua tu kupitia Adamu. Kwa mujibu wa ushuhuda wa Biblia, huenda alikuwa amelisikia kupitia Adamu tu wakati Shetani alipomshawishi kuivunja amri; kwa maana alipolirudia agizo hilo, alipamba maneno, akaifanya sheria kuwa kali zaidi katika jambo moja na dhaifu zaidi katika jambo lingine – na hizo ni dalili za habari iliyosimuliwa kwa kusikia kutoka kwa mwingine, si ya taarifa ya moja kwa moja. Hatimaye wote wawili walikula matunda ya mti huo, na Mungu akaja wakati wa jua kupunga ili kuwahoji. Akamwuliza Adamu: “Je, umekula matunda ya mti ule?” na jibu lilikuwa: “Huyo mwanamke ULIYENIPA awe pamoja nami, YEYE ndiye aliyenipa matunda ya mti, nikala.” Kisha Mungu akamwuliza mwanamke, naye akajibu: “NYOKA alinidanganya, nikala.” Tafadhali angalieni maneno niliyoandika kwa herufi kubwa.

69 Kwa maoni yangu ni haki kulinganisha majibu haya mawili, kwa maana ndani yake tunapata dokezo la yale yanayofuata. Wote wawili wanakiri: “Nilikula”, na wote wawili wanataja kwa ukweli msukumo wa *moja kwa moja* uliowafanya wale. Mpaka hapo wako sawa. Lakini Adamu anaona kwamba analazimika kusema zaidi. Kulikuwa na chanzo cha kwanza cha anguko lake kupitia Hawa: Shetani. Lakini Adamu hamtaji Shetani kama Hawa alivyomtaji; wala hanyamazi kuhusu chanzo cha kwanza; anamshtaki Mungu moja kwa moja usoni pake kuwa yeye mwenyewe ndiye chanzo hicho cha kwanza – kwa kumpa mwanamke. Na baya zaidi ni kwamba Shetani alikuwapo katika mazungumzo hayo au karibu, wala hangeweza kupuuzwa, isipokuwa kwa makusudi, ikiwa ilikuwa lazima kutaja chanzo cha kwanza. Shetani lazima alifurahi kuhusu mtazamo wa Adamu kwa Mungu, na kwa kuwa alimshtaki Mungu kwa njia isiyo ya moja kwa moja kuwa na upumbavu, kama vile alivyofurahi kuhusu mtazamo wa Adamu kwake yeye mwenyewe, mjaribu, kwa sababu alimtetea dhidi ya mashtaka. Je, si tukio hili, mwenendo huu wa Adamu, ndio Ayubu anaourejelea (Ayubu 31:33) anapolalamika: “Kama nimefunika makosa yangu kama Adamu, kwa kuuficha uovu wangu kifuni mwangu ...”? Dk. Lange anasema (taz. aya ya 36): “Adamu alipaswa kuilinda na kuitunza [bustani] dhidi ya nguvu ya uovu iliyokuwapo.” Je, labda hii si sababu kwa nini Adamu hamtaji Shetani, ambaye aliweza kupata njia ya kuingia?

“Adamu alimshtaki Mungu moja kwa moja usoni pake kuwa yeye mwenyewe ndiye chanzo cha kwanza cha anguko – kwa kumpa mwanamke.”

70 Hatima ni neno la kutisha. Majaliwa ya mtu yanaweza kuamuliwa kwa maisha yake yote kwa uamuzi wa kitambo kimoja, na uamuzi huo unaweza – isipokuwa mtu amwombe Mungu aingilie kati – kuwa mwelekeo wa asili wa uzao wake katika vizazi vinavyofuata. Katika Maandiko hilo ndilo somo la Waisraeli na Waedomu. Maisha ya Esau yalionekana kuwa ya heshima zaidi kuliko maisha ya Yakobo, mpaka hatua fulani katika historia ya Yakobo. Lakini Esau aliposimama kwenye njia panda, alichagua kuburudisha mwili kwa gharama ya haki yake ya mzaliwa wa kwanza (Mwanzo 25:29-34). Baadaye sana Yakobo alifika kwenye njia panda, na hata kwa hatari ya kushambuliwa ghafla akiwa peke yake na bila kujiandaa na shambulio la kuua la ndugu yake, alishindana usiku kucha ili apate baraka ya Mungu (Mwanzo 32:24-32), akaipata. Hata kabla ya kuzaliwa kwa hawa wawili Mungu aliona aina ya maamuzi ambayo kila mmoja angefanya, akafanya “uchaguzi” wake kwa kufuata ujuzi huu wa mbele. Sasa Mungu – safari hii kwa msingi wa maamuzi ya Adamu na Hawa – yuko karibu kufanya “uchaguzi”, sawasawa na wakati ule, baadaye katika historia, alipomchagua Yakobo kuwa baba wa ukoo wa Masihi atakayekuja.

71 Adamu alifanya uamuzi mbaya. Alisimama upande wa nyoka akawa mchongezi wa Mungu. Lakini Hawa aliifunua tabia ya Shetani mbele yake mwenyewe, na hivyo akaweka uadui kati yake na yeye. Kilichofuata kilikuwa matokeo ya asili ya uchaguzi bora wa Hawa. Mungu aliamua kumvuta mwanamke

mbali zaidi na Shetani. Akamwambia Shetani: *“Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke”* (3:15). Kwa maneno mengine alisema: *“Yeye ameamua kufanya mfarakano; nami nitaupanua mfarakano huo.”*

Mengi yamekwisha kusemwa kuhusu ahadi tukufu inayofuata sasa, lakini na tusimame kidogo tukumbuke kwamba wafasiri kadhaa hawaoni ndani yake maana zaidi ya kwamba daima kutakuwa na uadui wa asili kati ya mwanadamu na mnyama wa hali ya chini, nyoka!

72 Hatupaswi kusahau kwamba wakati huo Mungu aliweka uadui kati ya Shetani na mwanamke. Hilo linaeleza kwa kiasi kikubwa mfululizo mzima wa maovu yanayotabiriwa katika mstari unaofuata (3:16), ambayo kwa mtazamo wa kimapokeo, bila shaka, ni matokeo ya kwamba Hawa aliingiza dhambi ulimwenguni kwa kula tunda lililokatazwa na kumpa mumewe pia. Uadui wa Shetani ndio chanzo cha mateso ya mwanamke. Nuru zaidi juu ya jambo hili itafuata katika masomo yajayo.

73 *“Na kati ya uzao wako na uzao wake”*, Mungu anaongeza kwenye maneno haya aliyomwambia Shetani kuhusu mwanamke. Licha ya msisitizo wa kawaida leo juu ya *“ubaba wa Mungu kwa watu wote”* na *“undugu wa wanadamu wote”*, ambao kwa sehemu ni kweli, sisi tunaoyaheshimu Maandiko kama mamlaka hatupaswi kusahau kwamba Shetani pia, kama Mungu, ana watoto wake – wakosaji wa kimaadili na wa kiroho – kati ya wanadamu. *“Mbegu njema ni wana wa ufalme; na magugu ni wana wa yule mwovu.”* Katika Yohana 6:70 imeandikwa: *“Je! Mimi sikuwachagua ninyi Thenashara, na mmoja wenu ni Ibilisi?”* Wayahudi walipotangaza: *“Sisi tunaye Baba mmoja, yaani, Mungu”*, Yesu alijibu: *“Kama Mungu angekuwa ndiye Baba yenu, mngenipenda mimi. ... Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi”* (Yohana 8:41-44). Hata mtume wa upendo, Yohana, hasemi kwamba watu wote ni watoto wa Mungu, bali anaonya: *“Watoto wadogo, mtu asiwadanganye; atendaye haki ni mwenye haki, kama yeye alivyo mwenye haki; atendaye dhambi ni wa Ibilisi, ... Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi”* (1 Yohana 3:7-8, 10). Mungu hawapokei wala hawatambui watoto *“wa haramu”* (Waebrania 12:8) wasiofanywa upya wa kanisa lililoanguka kuwa watoto wake.

74 *“Yeye [uzao wa mwanamke] atakuponda kichwa, nawe utamponda kisigino.”* Katika tafsiri za zamani kuna neno lenye maana ya amri (*“soll”*), lakini kwa ajili ya uwazi, mahali pote pawili lazima pawe na wakati ujao (*“wird”*). Ni maumbo ya wakati ujao, si amri. Mungu hamwamuru Shetani kuponda kisigino cha uzao wa mwanamke; anatabiri tu kwamba mambo haya yatatokea. Unabii huu unamhusu hasa adui mkuu wa Shetani, Yesu Kristo, aliyezaliwa na bikira Mariamu; lakini unawahusu pia waamini wote, kwa maana mtume Paulo anasema (Warumi 16:20): *“Na Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi”*. Tutaendelea na jambo hili katika somo letu lijalo.

Somo la 11 – HAWA NA WANAOMCHAFUA

82 Kama ukubwa wa kitabu hiki ungeruhusu, ningeweza kuongeza kwenye maelezo ya kasisi wa kanisa kuu Payne-Smith michango ya kuvutia ya wafafanuzi wengine wanaoshughulikia imani ya Hawa kwamba Kaini ndiye aliyekuwa Yule Ajaye, Masihi. Ya thamani hasa ni maelezo ya Dk. Peter Lange, wa Chuo Kikuu cha Bonn, na mhariri na mtafsiri wake Dk. Tayler Lewis. Huyu wa pili anaandika: *“Kosa la Hawa la kutumia usemi huo kwa mtu aliyekuwa zaidi mfano wa Mpinga Kristo kuliko wa Mkombozi, halipaswi kutushtua sisi – ambao Mungu wa agano amefunuliwa kwetu kama Nafsi iliyo tofauti kabisa na kuu kupita yote – kiasi cha kuathiri tafsiri ya andiko. Ufinyu wa ujuzi wa Hawa, na labda ukosefu wake wa kutofautisha ipasavyo kati ya kilicho cha Mungu na kilicho cha kibinadamu, unaweka nguvu ya tumaini lake na ukweli wa ndani wa maneno yake katika nuru iliyo kali zaidi. Kama maneno yake*

yaliyohifadhiwa yasingekuwa na dokezo lolote la uzao wa mwanamke ulioahidiwa, bila shaka wanarationalisti wangelitaja jambo hilo kama ushahidi kwamba hangeweza kujua lolote kuhusu unabii kama huo, na kwamba kwa hiyo Mwanzo 3:15 na Mwanzo 4:1 lazima viliandikwa na waandishi tofauti ambao hawakujuana au walipingana.”

83 Si Adamu tu, bali hasa Neno la Mungu lenyewe linasema kwamba Hawa alikuwa *“mama yao wote walio hai”*. Delitzsch anasema kuhusu jambo hili: “Ahadi kweli inazungumza juu ya uzao wa mwanamke. Mbele ya kifo kinachomtishia, mwanamke kwa Adamu ni hakikisho la mambo yote mawili, kudumu na pia ushindi wa jamii ya wanadamu.” Kuhusu wazo kwamba waamini wote ni “uzao wa mwanamke”, Dk. Monroe Gibson anatoa maelezo kwa swali: “Uzao wake ni nani?”, naye anajibu: “Wasomaji wengi wasiosoma kwa makini wanadhani kwamba uzao wake ni wanadamu wote. Kwa maana fulani, bila shaka, wanadamu wote ni ‘uzao wa mwanamke’, lakini kama unajumuisha wanadamu wote, basi uzao wa nyoka unamaanisha nini? Je, si dhahiri kabisa kwamba ‘uzao wa mwanamke’ hauwezi kumaanisha wanadamu wote, bali tu wale ambao si kwa maana ya kimwili tu, bali kwa maana ya kiroho ni ‘uzao wa mwanamke’, wale walio upande wa mema, upande wa Mungu na wa haki? Wale walio na roho iliyo kinyume ni uzao wa nyoka, ‘watoto wa Ibilisi’. Vivyo hivyo, tunaposoma, *‘Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa, kwa kuwa alikuwa mama yao wote walio hai’* [3:20], wasomaji wengi wanaelewa kwamba alikuwa mama wa wanadamu wote. Lakini kwa nini ampe jina linalosema jambo lililo dhahiri hivyo? Kwa upande mwingine, ikiwa ‘walio hai’ wanaeleweka, kwa maana ya kiroho na pia ya kimwili, kuwa wale walio ‘hai kwa Mungu’, watakaokuwa na ‘uzima’ ambao Mungu anatoa kupitia Mwanawe, jinsi gani madokezo yote yanavyopatana vizuri! ‘Uzao wa mwanamke’, ‘mama wa walio hai’, ‘vizazi vya Adamu’. Kwa usahihi, katika Kiebrania hakuna wakati uliopo, ila wakati uliopita na wakati ujao tu. Kwa hiyo wakati ujao unapotumika, unaweza kumaanisha wakati uliopo unaoendelea hadi wakati ujao. Hivyo hapa haisemwi tu ‘nitaweka uadui’, bali pia: ninaweka uadui kati yako na mwanamke. Kazi imeanza ... Yeye ndiye mfano wa asili na mwakilishi wa watu wote binafsi wanaounda kanisa la Mungu.” (*The Ages before Moses*, uk. 122).

84 Sasa na tulinganishe vifungu vinne vya Biblia kati ya vingi ambavyo ningeweza kuchagua. Mungu anamwambia Ibrahimu (Mwanzo 22:16-18): *“Nimeapa kwa nafsi yangu ... katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umeitii sauti yangu”*. Kwa Isaka anasema: *“Katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa kuwa Ibrahimu aliisikia sauti yangu, akayashika maagizo yangu”* (Mwanzo 26:4-5). Kwa Yakobo alisema vivyo hivyo (Mwanzo 28:14). Kwa Daudi anasema: *“nitamwinua mzao wako baada yako ... nami nitakifanya imara kiti chake milele”* (1 Mambo ya Nyakati 17:11-12). Kisha, Wagalatia 3:29: *“Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, warithi sawasawa na ahadi.”* Je, ilikuwa heshima ya pekee kwa Ibrahimu, Isaka, Yakobo na Daudi kutajwa kama sehemu za mkondo huu wa baraka uliopaswa kuwashukia wanadamu? Basi ni vizuri tukumbuke kwamba chanzo cha baraka hii (kwa upande wa kibinadamu) ni Hawa, ambaye Mungu alimwambia Shetani kumhusu: *“Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke; ... uzao wake ... utakuponda kichwa”*. Ahadi hiyo inamheshimu Hawa sawa na Ibrahimu, Isaka na Yakobo, na heshima hiyo isingeweza kumjia kwa sababu nyingine yoyote isipokuwa ileile, yaani kwa sababu ya ubora ulioonekana ndani yake.

85 Katika somo letu lijalo nitaonyesha kwamba AJ inafundisha kwamba Adamu, si Hawa, ndiye aliyeleta dhambi, na mauti kwa njia ya dhambi, ulimwenguni. Lakini basi uchafuaji huu wa tabia ya Hawa unawezaje kuelezwa? Chanzo chake ni nini? Nadhani jibu la maswali haya ni rahisi kabisa. Kihistoria, shtaka la mwanzo kabisa lililo wazi dhidi ya mwanamke kama chanzo cha maovu yote ni hadithi ya kipagani ya Kigiriki ya Pandora. Kwa mujibu wa Hesiod, aliyeishi karibu mwaka 800 KK,

Jupiter alikasirika kwa sababu Prometheus (jina lake linamaanisha “kuona mbele”) alikuwa ameiba moto kutoka mbinguni, na kwa kulipiza kisasi akamwamuru Hephaistos amfanye mwanamke mzuri. Minerva alimpamba kwa vipawa vyote, naye akaitwa Pandora (maana yake “aliyepewa kila kipawa”), lakini Mercury alimpa roho ya udanganyifu. Akapelekwa kwa Epimetheus (“wazo la baadaye”), aliyempokea kinyume na maonyo, wakati Prometheus hayupo. Alipopokelewa kati ya wanadamu, Pandora alifungua chombo na kuyaachia maovu yote ya wanadamu yatoke, isipokuwa tumaini la udanganyifu. Kuna matoleo mengi ya hadithi hii, lakini yote yanafundisha mtazamo mmoja: Mwanamke ndiye chanzo cha maovu ya wanadamu.

86 Kipindi kati ya maagano, wakati kati ya AK na AJ, kilikuwa katika historia ya Wayahudi “wakati wa mchanganyiko”, kwa sababu Wayahudi walijitahidi kupatanisha mafundisho ya AK na desturi za Wayahudi na upagani wa Kigiriki. Shemasi mkuu Farrar³ anasimulia kwamba “Palestina wakati huo ilizungukwa na ukanda wa miji ya Kigiriki, ambamo Wayahudi wengi walichangamana kwa uhuru na wakazi wa kipagani. Katika Yerusalemu yenyewe kunakua chama tajiri na chenye nguvu, kilicho na uhusiano wa karibu na wafalme wa Kigiriki wa Shamu na Misri. Wakivutiwa na mvuto wa maisha ya Kigiriki na fasihi ya Kigiriki, walitaka kuchukua maadili ya Kiyunani na kufuta alama muhimu kabisa zinazotofautisha maisha na imani ya Kiyahudi. Kipindi hiki cha nusu-kutoamini kimeelezwa kama ‘siku za mchanganyiko’.”

87 Kwa hiyo si jambo la ajabu kwamba katika kipindi hiki yalifanyika majaribio ya kupatanisha hadithi ya Pandora na habari ya Hawa katika Mwanzo; na dokezo la zamani kabisa lililohifadhiwa kuhusu Hawa kama chanzo cha uovu linapatikana katika kitabu cha Apokrifa kinachojulikana kama *Ecclesiasticus au YOSHUA bin SIRA* (Yesu Siraki). Kitabu hiki, kazi ya Kipalestina ya tarehe isiyojulikana, hapo awali kiliandikwa kwa Kiebrania, labda karibu mwaka 250 KK, lakini mapema kilitafsiriwa kwa Kigiriki huko Misri, na kina maneno haya: “Kutoka kwa mwanamke ulikuja mwanzo wa dhambi, na kwa sababu yake sisi sote tunakufa.” (25:24). Tennant anasimulia kwamba “Yesu Siraki alikuwa mtangulizi wa fundisho la Talmud kuhusu anguko”.⁴ Hivi punde nitaonyesha kwa kunukuu sehemu kile ambacho fundisho hilo la Talmud linasema kuhusu Hawa, – kwa hiyo tafadhali msilisahau jambo hili.

“Dokezo la zamani kabisa lililohifadhiwa kuhusu Hawa kama chanzo cha uovu linapatikana katika kitabu cha Apokrifa kinachojulikana kama Ecclesiasticus au YOSHUA bin SIRA.”

Waandishi wa Kiyahudi wa baadaye wanaeleza kwa undani zaidi hatia ya Hawa. Hasa huko Aleksandria lilifanyika jaribio la kupatanisha Maandiko Matakatiifu na mafundisho ya kipagani ya Kigiriki. Kwa hasara ya theolojia ya Kikristo, baada ya kukamilika kwa toleo la Kigiriki la AK huko Aleksandria (lililoanzwa mwaka 285 KK), maandiko haya ya Kiyahudi yasiyovuviwa, yaliyoitwa “Apokrifa” – yote yameandikwa kwa Kigiriki, si kwa Kiebrania – yaliingizwa katika toleo hilo, ambalo kanisa lilitumia bila maandiko ya Kiebrania. Mababa wengi wa Kanisa waliinukuu Apokrifa kana kwamba ina mamlaka; na wote waliathiriwa na mafundisho yake. Na hivyo inatokea kwa urahisi kwamba tabia ya Pandora wa hadithi za kale inahusishwa na Hawa. Hakuna usemi wowote kuhusu tabia ya Hawa unaoweza kufuatiliwa nyuma zaidi kuliko “siku za mchanganyiko”.

88 Irenaeus, askofu wa Lyon mwaka 177 BK, kwa kupatana na fundisho la Ben Sira na Wayahudi wengine, anasema kuhusu Hawa: “Kwa kuwa alikuwa amehisi, alifanywa kuwa chanzo cha mauti, kwa ajili yake mwenyewe na pia kwa ajili ya wanadamu wote.” Lakini miaka michache baadaye Tertullian wa Karthago ni mkali hasa; anawapatiliza wanawake wote Wakristo dhambi ya Hawa, kwa maneno haya: “Na wewe hukutaka kujua kwamba wewe ni Hawa? Hukumu ya Mungu juu ya jinsia yako bado inaendelea kuishi katika ulimwengu huu; basi lazima hatia yako nayo bado inaendelea kuishi. WEWE

NDIWE ULİYEMFUNGULIA IBILISI MLANGO, wewe ulivunja muhuri wa mti ule, wewe ulikuwa wa kwanza kuiacha sheria ya Mungu, wewe pia ndiwe uliyemdanganya yule ambaye Ibilisi hakuweza kumkaribia. Kwa urahisi hivyo ulimwanguka chini mwanamume, mfano wa Mungu. Kwa sababu ya hatia yako, yaani kwa sababu ya mauti, hata Mwana wa Mungu ilimbidi afe.” Lakini je, bila mwanamke, wanadamu wangewahi kuona Mwana wa Mungu akija ulimwenguni ili kufa au kuwahubiria wanaume?

89 Mitazamo mingi ya kitheolojia katika wakati wetu inashuhudia mkono wa Tertullian ulioiunda, kwa maana, kwa kutumia maneno mafupi ya *Lippincott’s Biographical Dictionary*: “Alipata ushawishi mkubwa kati ya Wakristo wa wakati wake”. Kazi zake nyingi za maandishi zimehifadhiwa hadi leo. Mtu akianza na mtazamo kama huo kuhusu mwanamke (kwamba kwa sababu ya ‘hatia’ ya kudumu ametengwa asishiriki manufaa ya dhabihu ya upatanisho ya Kristo kwa ajili ya dhambi), si ajabu kwamba andiko linalofuata tutakaloliangalia (Mwanzo 3:16), kwa kupatana na fundisho la Talmud na la Tertullian, limefasiriwa kuwa laana ya milele ya Mungu juu ya jinsia yote ya kike.

Somo la 46 – VISINGIZIO VISIVYO VYA LAZIMA KWA AJILI YA MANTIKI YA PAULO

346 Basi, tuna mbadala gani wa mtazamo huu kwamba Paulo anatoa ushauri unaofaa kwa ajili ya dharura kubwa – na kwamba *hatetei* ukimya wa kudumu na unyenyekevu wa mwanamke? Kwa mujibu wa wafafanuzi, inafikia kusema kwamba mtume, ambaye kwa upande mmoja alitumia muda mwingi hivyo kupiga vita “hadithi za Kiyahudi” za Wayahudi-Wakristo walioshika sheria (Judaisti), kwa upande mwingine yeye mwenyewe aliathiriwa sana na shule hiyo hiyo, – kwa maana maelezo hayawezi kuepukika kwamba Paulo hapa anatumia kwa ukarimu hila za hoja za Kiyahudi zisizo za kuaminika, isipokuwa tufikie hitimisho kwamba *wengine* wameyachanganya mafundisho ya Paulo na hila za hoja za kujinufaisha. Calvin kwa mfano anaandika kuhusu hoja, “Adamu aliumbwa kwanza”: “Lakini sababu ambayo Paulo anaitoa, yaani kwamba mwanamke alikuwa wa pili katika mpangilio wa uumbaji, haionekani kuwa hoja yenye nguvu sana kwa ajili ya unyenyekevu wake, kwa maana Yohana Mbatizaji alikuwa kabla ya Kristo kwa mpangilio wa wakati, lakini alikuwa chini yake sana kwa cheo”, – naye Calvin angeweza kuongeza: “Kila mwanamume ana mama aliyeumbwa kabla yake, lakini mama huyo anahesabiwa kuwa duni.” Au, ikiwa Paulo alirejelea tendo la asili la uumbaji: “Ng’ombe waliumbwa kabla ya wanaume – hata kabla ya wanatheolojia, – kwa hiyo wanaume lazima wawe chini ya ng’ombe.” Mimi kwa upande wangu niko tayari zaidi kudhani kwamba mfafanuzi ndiye aliyetumia hila za hoja zisizostahili, kuliko kuamini kwamba Paulo alifanya hivyo.

347 Tukifuata mtazamo kwamba Paulo analazimisha mafundisho ya marabi, basi, kama Kalisch anavyoandika, “Agano Jipya ... ni kali zaidi kuliko la Kale; kwa maana wakati linamwamuru mwanamke ajifunze katika utulivu kwa unyenyekevu wote, lakini asifundishe wala asidai mamlaka juu ya mwanamume, bali anyamaze’, katika Agano la Kale aliruhusiwa kushika kazi ya juu kabisa ya kufundisha, ile ya manabii, kama Miriamu, Debora na Hulda.” Hata hivyo ningeamini zaidi kwamba mfafanuzi amekosea, kuliko kwamba neno “Injili” – “Habari Njema” – linawatangazia wanawake ukandamizaji ambao haukulazimishwa kwao chini ya sheria ya Agano la Kale.

348 Wakati mwingine mfafanuzi, akiridhika na *maagizo* ya Paulo lakini akiwa na wasiwasi kuhusu *namna yake ya kujenga hoja*, anajaribu kumtetea Paulo kwa visingizio. Prof. Reynolds anasema kuhusu mstari wa 13: “Hoja hii inaweza kusikika kwetu kuwa imetafutwa mbali sana, inapotumika kukataa madai ya kike ya ubora wa kiakili. Hata hivyo wakati huo ilikuwa njia ya kawaida kutafuta na kupata katika Maandiko kielelezo halisi cha karibu kila mtazamo wa kifalsafa.” Hilo linasikika kuwa la busara sana. Lakini nimezoa kuamini kwamba Roho Mtakatifu ndiye aliyeyaongoza maandiko ya Paulo; na

siamini kwamba Roho alihitaji kujifunza upuuzi wa marabi ili kupata sababu ya kuhalalisha ukimya na unyenyekevu wa wanawake. Ukosefu wa sababu za busara kweli ungekuwa mbaya kabisa, kabla Paulo hajaridhika na hoja kama zile anazohusishwa nazo hapa!

349 Mtume ambaye kwa mantiki yenye nguvu aliandika Waraka kwa Warumi, na ambaye ama aliandika hoja zilizo wazi za Waraka kwa Waebrania au alikuwa mwalimu wa yule aliyeziandika, hakuhitaji kurudi kwenye kitu ambacho yeye mwenyewe kwa dharau alikiita “hadithi za Kiyahudi” – na ambazo alimwonya Timotheo aziepuke –, ili kupata kisingizio cha kuwanyamazisha wanawake. Kama angetaka kuwanyamazisha, angekuwa na sababu ya kweli ya kufanya hivyo, na angeweza kupata lugha inayofaa kueleza sababu hiyo. Jukumu zito liko juu ya wale wanaomfanya Paulo kuwa kitu cha dhihaka na Biblia kuwa kitu cha mashaka kuhusu thamani yake, kwa kujaribu kushikilia hila za hoja kwa visingizio dhaifu kwa ajili ya Paulo. Sitakubali hata kwa kitambo kimoja kwamba mtume, wala Biblia kwa jumla, wanahitaji kutetewa kwa visingizio. Mara wafafanuzi watakapokuwa tayari kuacha jaribio la kuthibitisha mahitimisho ya ubinafsi yaliyokwisha kuamuliwa kabla, maneno ya Paulo yatakuwa wazi kabisa na yenye mantiki kwa maana ya Kikristo. Nimeonyesha kwamba Paulo hakutetea unyenyekevu wa mwanamke chini ya mwanamume; wala kwamba Hawa alikuwa na hatia zaidi kuliko Adamu. Alipendekeza tu “utulivu” wa muda wa wanawake katika kanisa, kwa kuwa kulikuwa na hatari ya pekee kwa kanisa na kwa mwanamke katika hali ngumu. Mateso ya Nero yalikuwa yakiendelea, na usafi wa wanawake Wakristo ulikuwa hatarini.

“Kama Paulo angetaka kuwanyamazisha wanawake, angetaja sababu ya kweli ya kufanya hivyo, na angepata lugha inayofaa kueleza sababu hiyo.”

350 Hata hivyo Prof. Ramsay anaendelea kushikilia hitimisho kwamba Paulo alitaka kuwanyamazisha wanawake wote na kuwaweka chini nyakati zote, na (katika *The Expositor*, 1909) anaiita lugha ya Paulo mahali hapa

“... mfano wa ajabu wa jinsi Wayahudi kwa kawaida walivyotoa hoja kutoka katika Maandiko, na kuyapotosha na kuyatesa maneno yake ili kuunga mkono maoni waliyoyashikilia. Hata pale ambapo Paulo anaeleza kweli anayoiona wazi kwa ufahamu wa moja kwa moja usio na kosa, wakati mwingine anachukua kutoka Agano la Kale hoja ambazo kwetu zinaonekana zimesokotwa sana, na kama hoja hazina thamani kubwa. Fikira za Kiyahudi zilijenga hoja kwa njia tofauti kabisa na sisi; na kwa mwelekeo wake wa hoja mara nyingi zinatushangaza. Lakini hatupaswi kulinganisha ukweli wa mtazamo na uhalali wa hoja, wala kufikia hitimisho kwamba, kwa sababu hoja haishawishi sana, kwa hiyo mtazamo huo si kweli. Kwa hiyo tunaweza kuiweka kando hoja inayotokana na mwenendo wa Adamu na Hawa, kama isiyovutia fikira zetu na isiyoieleweka kwetu kwa urahisi. Na kwa kadiri inavyoeleweka, katika hukumu ya wasomaji wa kisasa haiwezi kuimarisha lengo la Paulo. Lakini lengo lake halitegemei hoja hiyo hata kidogo.”

351 Nafurahi sana kwamba “katika hukumu ya wasomaji wa kisasa” jambo la unyenyekevu na ukimya wa wanawake halijaimarishwa na hoja ambayo Paulo *anahusishwa* nayo, kwa maana sasa napata tumaini kwamba mfafanuzi hivi karibuni atatambua kwamba hoja dhaifu namna hiyo haitoki kwa Paulo hata kidogo, bali ni kazi ya wapotoshaji wa maneno ya Paulo. Si Paulo aliyeyapotosha Maandiko, bali wanaume wamezipotosha hoja za Paulo zisipatane na Maandiko. Lakini kuna tumaini, wafasiri wakianza tu kutambua upotoshaji katika lugha. Prof. Ramsay anadhani kwamba hoja ya Paulo ni mbaya, lakini kwamba hitimisho lake kutoka kwa hoja mbaya ni la kweli. Lakini mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri. Ikitambuliwa tu kwamba utawala wa mwanamume juu ya mwanamke ni kama

mali iliyopatikana kwa hati ya umiliki yenye kasoro, wanaume hawawezi kupigana dhidi ya dhamiri zao zenye hatia; na mwanamke anaye Mungu upande wake. Kutokana na hili tunahitimisha: Kati ya njia hizi mbili – ama (1) kukubali kwamba Paulo alitetea jambo tofauti kabisa, au (2) kudai kwamba Paulo alijenga hoja kwa udanganyifu kwa kuyapotosha Maandiko (ili kutetea ukimya na unyenyekevu wa mwanamke) – ni heshima zaidi sana kwa Paulo, na ni kicho zaidi kwa Mungu na kwa Neno Lake, kuukataa mtazamo wa pili na kuukubali wa kwanza.

352 Nimeonyesha kwamba katika maneno ya Paulo kwa Timotheo kuhusu wanawake kuna maana inayopatana na inayofaa, kinyume kabisa na wazo kwamba anaendeleza hila za hoja za marabi. Hata hivyo Prof. Ramsay, bila kunukuu mitazamo mingine ya namna hiyo, anamshtaki Paulo kwa “namna ya kujenga hoja iliyosokotwa na ya ajabu” ili kuunga mkono fundisho (lililochukuliwa kutoka kwa marabi) kwamba mwanamke yuko chini ya mwanamume. Hakuna anayeweza kukana kwamba namna ya kujenga hoja iliyosokotwa na ya ajabu imetumika ili kulazimisha fundisho kama hilo kwa msaada wa andiko hili la Timotheo. Hilo ni dhahiri. Lakini ninakana kwamba Paulo ndiye mwenye hatia ya Neno la Mungu kupotoshwa. Ninaona hatia iko kwa “Judaisti” ndani ya kanisa la kwanza; na wafafanuzi wanaume, kwa sababu za kujinufaisha (labda bila kujua), wamechukua hoja hii iliyokwisha kuandaliwa, iliyosokotwa na ya ajabu ya “Judaisti”, ambao ushawishi wao mbaya kwa kanisa Paulo mwenyewe aliupiga vita kila siku katika huduma yake yote. Alionya juu yao na kutabiri kuhusu wao hivi: *“Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi”* (Matendo 20:29). Aliwalaumu wao na mafundisho yao mara nyingi sana katika nyaraka zake kadhaa; na baada ya Paulo, Petro aliwaonya Wakristo juu ya wale wanaoyapotosha maneno ya nyaraka za Paulo “kwa uvunjifu wao wenyewe” (2 Petro 3:15-16).

353 Paulo anasema kuhusu yeye mwenyewe katika 2 Wakorintho 4:1-2: *“Kwa sababu hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii, ... [sisi] tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo.”* Kwa hiyo, ili kukubali mtazamo kwamba Paulo aliangukia “hoja iliyosokotwa na ya ajabu”, kama ile iliyowatambulisha “Judaisti” wa siku zile, tunapaswa kuamini mengi zaidi kuliko tu kwamba Paulo “aliipotosha na kuitesa lugha ya Maandiko” (kwa kutumia maneno ya Prof. Ramsay). Tunapaswa kuamini kwamba Roho Mtakatifu, aliyeyavuvia maandiko ya Paulo, alimpisha roho ya uongo, na kwamba Paulo, alipoandika usemi huu kuhusu yeye mwenyewe, hakuwa mkweli; lakini mimi sina maoni kama hayo kuhusu Paulo.

Somo la 47 – MANENO YA MWISHO KUHUSU UKICHWA WA MUME

354 Basi, ikiwa ukichwa wa mume haumaanishi utawala wa mwanamume, kwa nini mke anaagizwa “kumnyenyekea” mumewe, na si mume kumnyenyekea mke wake? Kwa sababu maana halisi ya neno “unyenyekevu” haihusu utumwa, bali kupatana (upatanisho kati ya watu). Mahali ambapo dhuluma inatawala au inashukiwa, njia ya Kikristo daima ni kumhimiza yule anayeonewa ajitahidi kutafuta amani, ikiwezekana, mpaka mkosaji atakapojifunza vizuri zaidi. Someni 1 Petro 2:18-23 kuhusu jambo hili: Angalieni mpito kwenda 3:1, hasa neno “vivyo hivyo”. “Unyenyekevu” unaodaiwa unahusu mume mkaidi asiyeamini. Vivyo hivyo mtume Paulo katika Waefeso 5 anamhimiza mke, ambaye ndiye kwa kawaida huteseka kwa dhuluma, kwenye mfululizo wa wajibu unaojumlishwa katika neno “unyenyekevu”, na mume kwenye mfululizo mwingine wa wajibu, kwa sababu yeye ndiye mwenye mwelekeo zaidi wa kukandamiza. Mume anapaswa kuonyesha upendo ule unaojitoe kwa ajili ya mema ya mwingine.

355 Lakini mfafanuzi anaielewa vibaya *nia* ya Paulo anapotumia neno “unyenyekevu”. Jambo hilo linaweza kuelezwa kwa mfano huu: Huko China, kwa karne nyingi akina mama wamejiona kulazimika kuifunga miguu ya wasichana wao ili kuwaandaa kwa ajili ya soko la ndoa. Desturi hii sasa inaachwa kwa sababu ya mvuto wa utu wa dini ya Kikristo, na akina mama, wakiungwa mkono na wanaume wa familia zao, wanakataa kuifunga miguu ya binti zao, na mara nyingi wanafungua bendeji za miguu yao wenyewe. Lakini kuwa na miguu huru ni jambo *moja* kwa binti ambaye miguu yake *haijawahi* kufungwa, na ni jambo tofauti kabisa kwa mama ambaye miguu yake *imefungwa kwa miaka mingi*. Sababu ni kwamba bendeji zile zile zilizoifanya miguu kuwa dhaifu na kilema, baada ya muda zimekuwa *tegemeo la lazima* kwa viungo vilivyodhoofika; kwa hiyo daktari mmisionari wa kike, anapoifungua miguu ya mama wa Kichina, anapaswa kuondoa bendeji za zamani *kisha kuweka bendeji mpya*, – safari hii kwa kufunga kila kidole kwenye banzi lake binafsi, – kwa muda tu, mpaka mguu utakapoweza kuachiliwa kutoka kwa kila tegemeo.

356 Kitendo hiki cha pili kweli ni kitendo cha kufunga, lakini kinafanyika kwa *nia iliyo kinyume kabisa* na ile ya kufunga miguu hapo awali. Kinahusu kurudisha uhuru uliopotea, wakati kitendo cha zamani kiliuiba uhuru kwa ukali na kwa kushambulia. Zaidi ya hayo, kwa asili yake ni kitendo kisichofaa kabisa kwa msichana ambaye miguu yake haijawahi kufungwa. Je, sasa ingekuwa haki au kweli, kwa sababu ya *matibabu haya ya muda* yaliyofanywa na daktari, yanayolenga uhuru kamili, kudhani kwamba daktari anaona kufunga miguu kuwa jambo la faida? Lakini hasa kwa maana hiyo Paulo ameeleweka vibaya na wale wanaotaka kuhalalisha utawala wa wanaume. Wanapuuza lengo la Paulo alilolitangaza; wanakaa kimya mbele ya maneno yake yaliyo wazi mahali pengine kuhusu “*uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu*”; wanadharau maonyo ambayo Paulo anayatumia kuyalinda maneno yake, na kuipotosha maana yake.

357 Maneno kama “*Hakuna Myahudi wala Myunani, hakuna mtumwa wala huru, hakuna mtu mume wala mtu mke*” kwa uelewa wao yana mamlaka kidogo tu; lakini kwa sababu Paulo alimkumbusha mwanamke mara mbili kwamba mume wake ni “kichwa” chake (“tegemeo”, taz. aya ya 282), wafasiri hawa wanataka kuwatwika wanawake tena kwa kudumu mizigo ya ukandamizaji ambayo Paulo alitaka kuiondoa kutoka migongoni mwao iliyopinda. Maelezo haya potofu ya nia ya mtume yamewafanya watu wengi kuidhihaki Biblia na Paulo bila heshima; na jukumu la hilo ni la wale wanaopotosha kile Paulo alichomaanisha. Paulo hasemi kama “mseja mzee mwenye uchungu”, bali kama msemaji wa Mungu. Wala hafanyi kazi chini ya pumzi yenye sumu ya mafunzo ya kirabi. Paulo anasema chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, na anaweza kueleweka kwa urahisi, kwa msaada wa Roho, na wale wanaotaka kumwelewa sawasawa. Kila maelezo mengine ya maneno yake ni ya kukosa heshima.

358 Mtume, akitambua magumu chini ya serikali ya kipagani na chini ya sheria za kiraia zisizo za haki kwa wanawake, sasa kwanza anaeleza kwamba ndani ya kanisa bendeji za ukandamizaji lazima ziondolewe, lakini kwamba kifungo cha ndoa lazima kihifadhiwe kwa uangalifu (“*Ndoa na iheshimiwe na watu wote*.”); wake lazima wawe na subira; na waume lazima, ili tubaki katika mfano ule, wawe kana kwamba ni banzi binafsi kwa kila mwanamke aliyevunjika na kupondeka. Maadili ya kimapinduzi ya upendo wa Kikristo yangeleta mengine yote kwa muda mfupi. Kama Bwana wake, Paulo alikuja kwa Injili yake “*kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao*”, – si kuwatangazia wafungwa kifungo. Lengo la Paulo kwa wanawake, kama kwa wanaume, ni “*uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu*”, naye analieleza tena na tena kwa njia nyingi; na mara lengo hili litakapofikiwa na wanawake, *njia* hiyo imepitwa na wakati na haina maana tena. Katika nchi za Kikristo, katika nyumba za Kikristo za kweli, maagizo ya pekee kwa mke “kumnyenyekea” mumewe hayana nafasi tena, – njia hiyo imemaliza kazi yake; ukandamizaji umetoweka; uhuru umepatikana.

359 Sasa na tuangalie Waefeso 5, mstari wa 22: *“Enyi wake, [nyenyekeeni] waume zenu wenyewe, kama kwa Bwana.”* Angalieni kwanza kwamba maneno yaliyo katika mabano hayamo katika maandishi ya asili. Wake wanapewa wajibu uleule ambao katika mstari wa 21 tayari umewekwa juu ya Wakristo wote, na hilo halimaanishi kupanua wajibu wa mke hadi kipimo kisichojulikana, bali kuuwekea mipaka. Muundo wake unalingana na Wakolosai 3:18, ambapo tunakuta orodha ileile ya wajibu: *“... kama ipasavyo katika Bwana”*. Kwa Paulo, unyenyekevu ungeweza kuvuka kipimo cha kile *“kinachopasa”*. Kwa maana ndugu wa uongo walipomjia na kumpa ushauri mbaya, alitangaza: *“Hatukujitiisha kwao, wala hatukuwanyenyekea hata saa moja.”* Naam, mtume huyu, aliyewafundisha waamini wote *“kunyenyekana”*, kama alivyofanya Petro pia (1 Petro 5:5), anasema hata kuhusu Petro: *“nalishindana naye uso kwa uso, kwa sababu alistahili kulaumiwa”* (Wagalatia 2:3-5, 11). Unyenyekevu usio na mipaka kwa mtu mwingine haujawahi kuwekwa na Biblia juu ya Mkristo, awe mwanamume au mwanamke.

“Unyenyekevu usio na mipaka kwa mtu mwingine haujawahi kuwekwa na Biblia juu ya Mkristo, awe mwanamume au mwanamke.”

360 Mshairi John Milton anatetea fundisho tofauti kabisa kwa wanawake kuliko mtume Paulo:

*“To whom thus Eve, with perfect beauty adorn’d:
 ‘My author and disposer, what thou bidd’st
 Unargued I obey: so God ordains;
 God is thy law, thou mine; to know no more
 Is woman’s happiest knowledge, and her praise.”*
*[Ambaye Hawa, aliyepambwa kwa uzuri mkamilifu, alimwambia hivi:
 ‘Mwanzilishi wangu na mtawala wangu, lile unaloliamuru
 Nalitii bila kubishana: ndivyo Mungu anavyoagiza;
 Mungu ni sheria yako, wewe ni sheria yangu; kutojua zaidi ya hayo
 Ndio ujuzi wa furaha kuu wa mwanamke, na sifa yake.’]*

Fundisho kama hilo linamweka mwanamume mahali pa Mungu. Ni roho ya Mpinga Kristo, *“aketiye katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kwamba yeye ni Mungu”* (2 Wathesalonike 2:4). Pia linamfundisha mwanamke dhambi ile iliyo chukizo kuliko zote kwa Mungu, ibada ya sanamu.

361 Ikiwa mtume hawaagizi waume kama waume *“unyenyekevu”* kwa namna ya pekee, si kwa sababu nyingine ila kwa kuwa ana sababu ya kumkabidhi mume wajibu ulio muhimu zaidi. Katika mstari wa 23 wa sehemu hii ya Waraka kwa Waefeso anamwambia kwamba, kama Bwana wake, anapaswa kuwa kwa mke wake *“mwokozi wa mwili”*. Jinsi gani Paulo anatamani mke awe huru na asiye na hatia! Mstari wa 25 unafundisha kujikana kabisa kwa ajili yake, kwa kufuata mfano wa Kristo. Mstari wa 26: kuutakasa mwili wa mke wake kwa tabia yake ya kimwili iliyotakaswa na kufanywa takatifu, *“ili amtakase na kumsafisha”*, ili mwishowe aweze kumleta kwa Kristo *“bila kuwa na ila wala kunyanzi”* (mstari wa 27), – huru kutokana na kila madhara ya kimaadili yaliyosababishwa na mwenendo wake. Mstari wa 28 unamfundisha kumpenda mke wake kama anavyoupenda mwili wake mwenyewe, yaani kumlisha na kumtunza. Mwenendo ulio kinyume – ukandamizaji kwa tamaa – ni kumchukia. Mstari wa 31: Yeye (si mke) anapaswa kuwaacha wengine wote na kuambatana naye peke yake (taz. aya ya 45-64).

362 Karne pekee ya mwanamke katika kanisa la Kikristo ilikuwa wakati wa mitume na kidogo baada ya hapo. Prof. Ramsay, katika kitabu chake cha thamani *The Church in the Roman Empire*, anaandika:

“Aina ya Ukristo wa kanisa la ulimwengu wote na la ‘katoliki’ iliimarika katika kutopenda kwake umuhimu wa mwanamke na huduma yake ya hadharani. Kutopenda kuligeuka kuwa chukizo, na kuna uwezekano kwamba kutopenda huko kunarudi nyuma hadi karne ya kwanza, na kwamba kabla ya katikati ya karne ya pili kulikuwa kumeongezeka kuwa chukizo.”

Kadiri chukizo hili lilivyoongezeka, tunaweza kuwa na hakika kwamba kila juhudi inayowezekana ingefanywa ili kupata uhalali wa ukimya na unyenyekevu wa wanawake; na “Judaisti” alikuwa tayari kuleta njia hiyo, yaani kwa kuyakunja na kuyapotosha Maandiko, hasa maneno ya Paulo, ili yafundishe jambo kama hilo. Hapa tuna kwa maneno machache historia ya ile “hoja iliyosokotwa na ya ajabu”, inayowezesha kutoa mahitimisho yanayoonekana kutokana na hoja zilizotolewa na Paulo; hoja ambazo, zikisomwa sawasawa na kufasiriwa kwa akili isiyo na upendeleo, zingeongoza kwenye tathmini tofauti kabisa ya mtume Paulo na mafundisho yake kuhusu “swali la wanawake”.

“Karne pekee ya mwanamke katika kanisa la Kikristo ilikuwa wakati wa mitume na kidogo baada ya hapo.”

Somo la 66 – KUANZISHWA KWA FAMILIA YA KIKRISTO

519 Kwa mujibu wa mpangilio wa nyakati wa Agano la Kale unaotumika kwa kawaida (ule wa Usher), Ibrahimu alizaliwa mwaka 1996 KK, na Sara alikuwa mdogo wake kwa miaka kumi (Mwanzo 17:17). Kwa hiyo nyumba hii ya imani iliishi karibu kipindi kilekile kabla ya Kristo kama kile ambacho sisi tunaishi baada ya Kristo. Mpangilio huo huo wa nyakati unaweka wakati wa Hawa, ahadi ya uzao wenye ushindi ilipotolewa, katika mwaka 4004 KK, na hivyo unakadiria wakati wa Ibrahimu na Sara kuwa karibu katikati kati ya ahadi hiyo ya kukumbukwa na kuzaliwa kwa uzao wa mwanamke.

520 Tangu wakati wa Hawa hadi Ibrahimu (aliyeitwa *Abramu* mwanzoni), inaonekana Mungu hakuwa amehesabu uzao wa mwanamume kuwa sehemu ya ukoo wa Masihi ajaye. Wakati huo huo wanadamu, angalau katika sehemu ile ya dunia, walikuwa wamefuta desturi ya kuhesabu uzao kupitia nasaba ya kike; na mengi yaliyotambulisha heshima ya mwanamke ya nyakati za awali yalitoweka. Hata hivyo kwa njia fulani ilikuwa lazima njia ya Masihi ajaye iandikwe – zaidi ya ile kauli ya jumla kwamba angekuwa uzao wa mwanamke; na sasa nuru inaanza kupambazuka kuhusu taifa ambalo atakuwa sehemu yake atakapotokea. Wakati huo huo lilikuwa kusudi la Mungu kuliandaa taifa hilo ili limpokee.

521 Ibrahimu na mke wake Sara waliitwa waondoke kwa jamaa zao walioabudu sanamu (Mwanzo 12:1-5; Yohana 24:2-3). Walipofika Kanaani, Mungu alianza kuwalea kiroho, ili kuyainua matumaini yao hadi kiwango cha juu zaidi na kuyafunga kwenye uzao wao wa baadaye. Tutafanya vizuri kujifunza kwa makini maandalizi haya ya familia iliyokuwa ya kipagani, iwe kichwa cha nyumba zote za imani ya kweli kwa nyakati zote. Familia hii inaweza kweli kuitwa familia ya kwanza ya Kikristo, kwa maana ilifundishwa kumwamini Kristo ajaye (kama Hawa alivyofanya), – kama vile sisi tunavyomwamini Kristo aliyekuja na atakayekuja tena.

522 Mara nyingi tumeona jinsi majengo marefu sana yanavyojengwa, ambayo ni mengi katika miji mikubwa ya Amerika na ambayo leo yanazidi kuonekana pande zote mbili za bahari. Ujenzi wake ni tofauti kabisa na ule wa majengo madogo. Kwanza, udongo mwingi zaidi unachimbwa ili kupata nafasi ya msingi wenye kina na nguvu; kisha kila boriti na kila mhimili ni wa chuma, uliofungwa vizuri kwa

misumari ya chuma, kwa namna ya ujenzi wa madaraja. Mungu alitaka kuanzisha na kujenga nyumba ya kwanza ya imani kama kielelezo cha nyumba za Kikristo kwa nyakati zote. Alichimba kwa kina, akaweka imara mawe yake makubwa ya msingi, na kuzifunga pamoja vizuri boriti zote za jengo lake. Na tuchunguze jinsi alivyofanya.

523 Mungu anamwahidi Ibrahimu uzao mwingi kama nyota za mbinguni, na wakati huo huo hamruhusu Sara kuzaa hata mtoto mmoja. Alihitaji miaka mia moja ili kumwandaa Ibrahimu kuwa baba, na miaka tisini ili kumfanya Sara afae kuwa mama. *“Wasio haki ni kama makapi yapeperushwayo na upepo”*, asema Mungu, na *“Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili.”* Familia yenye heshima haijengwi juu ya makapi tu. Biblia inatufundisha: Mungu anapotaka uzao mwingi, anaweka mpangilio wa kuzaa watoto chini ya udhibiti wake mwenyewe. Kila kitu kinategemea ubora; familia kubwa ya Waishmaeli au Wafilisti si baraka kwa ulimwengu; na familia kama hiyo hata hivyo hudumu kwa muda mfupi tu; uovu, uhalifu na vita huifikisha upesi ukingoni mwa maangamizi.

524 *“Basi Sarai, mkewe Abram, hakumzalia watoto”* (Mwanzo 16:1). Kwa upande mmoja kulikuwa na ahadi ya *“uzao kama mavumbi ya nchi”* (Mwanzo 13:16), mwingi hivyo, kwa upande mwingine kulikuwa na mwanamke tasa. Hilo lilimaanisha nini? Hasa hili: Ubora ndio kila kitu kwa Mungu, hata kama wingi ndio lengo linalotakiwa. Huenda kwa Ibrahimu jambo lililotangulia lilikuwa hasa furaha ya kimwili juu ya uzuri wa Sara (Mwanzo 12:11-14), ambao nyuma yake ilivizia tamaa ya mwili iliyomfanya Abram wa kipagani amwoe dada yake wa kambo; kisha jambo hilo lilikuwa limechanganyika na kuangalia mbele, kulikovuviwa na uongozi na ahadi za Mungu, na Ibrahimu alitamani mrithi ambaye angemwachia utajiri alikuwa ameupata, na ambaye angeendeleza jina lake milele (Mwanzo 13:2; 15:3). Kisha Mungu akainua shauku zake hadi ulimwengu mzuri zaidi kuliko Kanaani – hadi *“mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu”* (Waebrania 11:10), na hatimaye, baada ya mwili wake kuwa *“umekufa”* kwa tamaa zote za kimwili (Warumi 4:19), mwana alizaliwa – kutokana na shauku takatifu ya kuubariki ulimwengu, kwa kutimiza ahadi ya Mungu kuhusu uzao wake (Mwanzo 12:3; 22:18). Shauku hii takatifu ililingana na shauku ya Mungu ya kuubariki ulimwengu kupitia Ibrahimu na Sara.

“Ubora ndio kila kitu kwa Mungu, hata kama wingi ndio lengo linalotakiwa.”

525 Jambo hili ni la kuangaliwa, na linatukumbusha kwamba Rebeka, Isaka alipomwoa, naye pia hakuruhusiwa kuzaa watoto mpaka tamaa ya mwili ilipoondolewa na shauku iliyo bora zaidi. Mrithi wa ahadi za Ibrahimu, Isaka, *“akamwomba BWANA kwa ajili ya mkewe, kwa sababu alikuwa tasa. BWANA akamjibu maombi yake”* (Mwanzo 25:21), – na hivyo Esau na Yakobo wakaja. Ahadi kwa Ibrahimu ya kuzibariki jamaa zote za dunia, katika hali yao, iliamishwa kwa Yakobo; na pia mke aliyechaguliwa na Yakobo, Raheli, hakuweza kuzaa watoto mpaka alipoomba kwa ajili ya jambo hilo; kitu kikubwa zaidi kuliko tamaa ya mwili au tamaa ya kibinadamu ya ukuu kililazimika kuhusika katika kuzaliwa kwa uzao wenye matumaini makubwa. *“Mungu akamkumbuka Raheli, akamsikia”* (Mwanzo 30:22), naye akamzaa yule ambaye hakuna kasoro iliyoandikwa juu ya tabia yake, Yusufu, mtu wa ajabu aliyeiokoa familia yake yote isife kwa njaa; wanawe, Efraimu na Manase, walikuwa wakuu wa makabila mawili ambayo yale manane mengine yalijikusanya kuyazunguka, na kuunda makabila kumi ya Israeli; hivi kwamba *“Israeli”*, tofauti na *“Yuda”*, mara nyingi huitwa *“Efraimu”* na manabii wa vipindi vya baadaye vya historia ya Agano la Kale (Yeremia 31:18 n.k.).

“Kitu kikubwa zaidi kuliko tamaa ya mwili au tamaa ya kibinadamu ya ukuu kililazimika kuhusika katika kuzaliwa kwa uzao wenye matumaini makubwa.”

526 Na ndivyo ilivyokuwa tena Mungu alipotaka mkombozi kwa ajili ya Israeli. Mama yake Samsoni *“alikuwa tasa, hakuzaa”*, na hatimaye malaika alipomtokea na kumpa maagizo kuhusu mtoto ajaye, tuna sababu ya kudhani kwamba yeye na mumewe walikuwa wameomba kuhusu jambo hili, – hasa kwa kuwa tunajua kwamba Manoa, baba yake, aliomba uongozi ulio wazi zaidi kuhusu malezi ya mtoto aliyetarajiwa (Waamuzi 13:8). Kisha tunafika kwa mtu yule mwenye tabia nzuri ajabu, mwanzilishi wa shule za manabii, Samweli. Alikuwa si kama jibu la tamaa ya mwili, bali kama jibu la maombi ya bidii ya Hana (1 Samweli 1:20). Mungu alimzuia (katika hali hii pia) asizae watoto mpaka shauku yake ilipotakaswa. Huenda hilo lilikuwa uzoefu wa akina mama wengine wengi, hata kama haukuandikwa hasa, walioza watoto mashuhuri katika nyakati za zamani.

527 Sasa tunafika kwenye Agano Jipya ili kujifunza somo lilelile kwa uzoefu wa Elisabeti. Mungu alikuwa karibu kumwandaa mtangulizi wa kuingia kwa Kristo ulimwenguni. Alichagua familia ya Zakaria na Elisabeti, na mara moja akaondoa uwezekano wa kupata mtoto wa mwili, ili Elisabeti aweze kuzaa mtoto aliyezaliwa kutokana na shauku takatifu isiyo ya tamaa ya kimwili. Alingoja muda mrefu – mpaka tamaa zote za mwili zilipokoma; kisha malaika akatumwa kuwatangazia: *“Usiogope, Zakaria, kwa maana dua yako imesikiwa, na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanamume ... Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana; ... atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye”* (Luka 1:13-15). Hivyo watu wakuu walizaliwa ulimwenguni, yaani watu walio wakuu mbele za Mungu, ingawa ulimwengu unaweza kuwadharau, kama Herode alivyomdharau Yohana Mbatizaji, kwa kumfunga gereza kwanza na kisha kumkata kichwa.

“Hivyo watu wakuu walizaliwa ulimwenguni, yaani watu walio wakuu mbele za Mungu, ingawa ulimwengu unaweza kuwadharau.”

Maelezo ya Ziada

Kuna tofauti kubwa sana ya kuangaliwa kati ya kusudi la Mungu katika kushughulika na wazazi hawa wa uzao mtakatifu, na malengo yanayofuatwa kwa vifaa vya kisasa vya “kudhibiti uzazi”. Hatua mbili za tamaa zinashindana ili kujidhihirisha, na Mungu anaamua kwamba kwa ajili ya uzao mtakatifu tamaa ya mwili ipite na mahali pake pachukuliwe na shauku ya kupata uzao, inayoonyeshwa kiroho katika maombi na dua. Kinyume chake, vifaa vya kisasa vilivyotengenezwa na wanadamu vitapunguza kuonyeshwa kwa shauku ya kupata uzao, na kuiachia tamaa ya mwili isiyowajibika ifanye kazi yake yote. Kwa kweli mtoto wa mahusiano ya namna hiyo angekuwa “wa uzao duni”, kama hatimaye angeruhusiwa kuzaliwa.

Somo la 100 – HAKI YA MZALIWA WA KWANZA AU CHAKULA CHA DENGU?

829 Fundisho lile la uongo linalotokana na “Laana Kumi za Hawa” za Talmud (taz. aya ya 106), kwamba Mungu huwaadhibu wanawake nyakati fulani kwa mateso kwa ajili ya dhambi ya Hawa, ni ushirikina mbaya na wa kikatili usiungwa mkono na Maandiko, na usiostahili akili zetu. Mwanzo 3:16 unatoa kifuniko kwa tamaa ya kimwili ya kiume yenye ubinafsi na unafiki ndani ya uhusiano wa ndoa, mstari huo unapopotoshwa na kusomwa kimakosa hivi: *“Tamaa yako na iwe kwa mumeo”* (Luther, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani). Zaidi ya hayo fundisho hilo ni picha potofu ya haki ya Mungu, kwa maana je, wanaume si wazao wa Hawa sawa na wanawake? Adhabu katika fundisho hilo haifuati dhambi, bali jinsia; na Mungu mwenyewe peke yake ndiye anayehusika na jinsia ya kila mtu.

830 Zaidi ya hayo, fundisho kwamba mwanamke lazima “anyamaze” kanisani daima, lazima amtii mumewe, na kamwe asithubutu kufundisha au kuhubiri, kwa sababu Hawa alitenda dhambi, linaharibu

fundisho la dhabihu ya upatanisho na kumnyang'anya Kristo heshima ya kwamba kifo chake kilifanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu wote, bila shaka pia dhambi za Hawa. Linapingana kabisa na roho ya Uprotestanti. Luther anasema: “Ni kosa kubwa kujitahidi sisi wenyewe kuitosheleza haki ya Mungu kwa ajili ya dhambi zetu, kwa maana Mungu huzisamehe daima bure kwa neema isiyopimika.”

831 Hata hivyo, ingawa inashangaza, Luther, kama wengine, anaonekana hakuwahi kuelewa wazo la “neema ya bure” kwa wanawake. Inasimuliwa kwamba alisema: “Kufa wakati wa kujifungua si kitu kingine ila kufa katika kazi tukufu na katika utii kwa Mungu. Hata kama wanawake wanajichosha kwa kubeba mimba na mwishowe kufa kwa ajili hiyo, hilo halidhuru. Waache tu wafe kwa kubeba mimba, ndiyo sababu wapo.” Luther alithamini sana “uhuru wa dhamiri”, lakini kuhusu wanawake alisema: “Hawezi kuanza wala kumaliza jambo lolote bila mume; alipo yeye, ndipo lazima awepo naye na kuinama mbele yake kama mbele ya bwana, ambaye atamwogopa na ambaye atakuwa chini yake na kumtii.” Hakuacha nafasi yoyote ya “uhuru wa dhamiri” kwa wanawake.

832 Luther si tofauti na mwelekeo wa jumla wa wafasiri wa Biblia. Huenda yeye ni mkali kidogo zaidi katika maneno yake kuliko wengine. Kwa bahati nzuri wanawake, walipoisikia “neema ya bure” iliyohubiriwa na wahubiri, wameipokea kwa ajili yao wenyewe. Na kinyume na kile kinachodhaniwa kuwa fundisho la Paulo, katika miaka ya karibuni wanawake wametwa moyo kushiriki katika mikutano ya hadharani ya makanisa, kwa sababu ilionekana kwamba mikutano bila wao ilikuwa ya kuchosha. Lakini kanisa lina haki gani kuunga mkono mwelekeo wa mafundisho ambao kwa matendo yake lenyewe linaupuuza? Je, si wakati sasa kwa kanisa ama kubadili matendo yake au kufuta mafundisho haya katika maelezo yake ya Biblia, na kwa njia moja au nyingine kuyapatanisha mambo haya mawili? Wajibu huu ni hasa wa wanawake, kuleta mapatano haya kati ya matendo yao wenyewe, yaani kushiriki katika mikutano ya hadharani, na mafundisho ya Biblia yanayodaiwa kwa kawaida.

833 Lakini tukiondoa katika imani yetu na katika mafundisho yetu wazo kwamba Mungu, kwa sababu ya dhambi ya Hawa, ameweka mkono wake wa kuangamiza juu ya jinsia yote ambayo Hawa alikuwa sehemu yake – basi fundisho kwamba ahadi ya uzao wa mwanamke utakaoponda kichwa cha nyoka ni ya wanawake wote linakuwaje? Tofauti ni hii: Unabii wa huzuni wa Mwanzo 3:16 umetimia kwa wingi kupita kiasi katika mateso na maumivu ya wanawake *yanayorithiwa kimwili*. Unabii mtukufu wa Mwanzo 3:15 nao utatimia kwa wingi kupita kiasi, lakini *si* kwa kurithi kimwili, bali kwa *uamuzi* wa hiari.

834 Unabii si majaliwa yasiyoepukika. Hakuna mwanamke aliyeamriwa tangu mwanzo kupata hatima tukufu ya kutimiza unabii huu, kwamba uzao wa mwanamke utaponda kichwa cha nyoka. Jambo hili halitanijia tu kinyume na mapenzi yangu – hivi kwamba niweze kujivunia kile kitakachokuja, vyovyote nitakavyofanya. Tunaambiwa tu kwamba *baadhi ya wanawake* watashika tuzo hii ya mwito wa juu wa Mungu katika Kristo Yesu; na nisipojiunga nao, kushushwa kwangu na adhabu yangu ya mwisho itakuwa kubwa zaidi, kwa sababu tuzo hiyo ilikuwa mbele yangu nami nikaidharau.

835 Kama nilivyokwisha kueleza, katika Biblia nzima hakuna dhambi inayowekwa wazi kwa dharau ya wanadamu kuliko ile ya Esau. Alikuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza mbele yake, na pamoja na haki hiyo, baraka ya kinabii ya baba yake. Lakini hayo yalikuwa mambo ya baadaye, ambayo kufika kwake kungeweza kuchelewa sana, wakati yeye alihisi hitaji la haraka la kushibisha njaa ya mwili. Angeweza kuwa katika ukoo ambao Kristo alikuja ulimwenguni kupitia kwake; lakini Kristo hakuja kwa muda mrefu bado, – naam, hakuja kwa karibu karne kumi na saba. Esau aliua haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa chakula cha dengu.

836 Agano Jipya linamwita yule *“asiyemcha Mungu, aliyeeuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja”*, na kuongeza: *“Maana mnajua ya kuwa hata alipotaka baadaye kuirithi ile baraka, alikataliwa”* (Waebrania 12:16-17). Baraka ya baba yake iliyomkalia yeye, mrithi wa haki ya mzaliwa wa kwanza, ingechangia sana ustawi wake wa maisha haya; lakini baada ya kuuza haki hiyo, hakuweza kuirithi baraka hiyo. Tendo hilo lilikuwa limefanyika zamani sana. Hapakuwa na nafasi tena ya kubadilisha. Alipata chakula cha dengi, lakini alipoteza sehemu mara mbili ya mali ya baba yake na nafasi ya heshima katika familia. Isaka asingeihamisha tena kwa Esau baraka ya mzaliwa wa kwanza aliyokuwa ameitamka juu ya Yakobo. Kwa maoni yangu, alikuwa ameelewa kwamba Esau alijali tu faida ya *maisha haya*.

837 Mtu asingeweza kuchora tofauti kubwa zaidi kuliko ile kati ya mwenendo wa Esau na mwenendo wa Musa, ambaye mwandishi yule yule wa Waraka kwa Waebrania anaandika juu yake: *“Kwa imani Musa, alipokuwa mtu mzima, alikataa kuitwa mwana wa binti Farao ... akihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri”*, zilizowekwa miguuni pake ili azifurahie (Waebrania 11:24-26). Fikirini! Huyu Musa mtukufu, aliyefundishwa hekima yote ya Wamisri, mwana wa binti mfalme! Anaacha yote na kusimama upande wa *watumwa wa Wamisri*! Ni mshupavu wa dini kiasi gani! Anamtazamia Kristo na kuutoa ulimwengu wote kwa ajili ya Kristo huyo, miaka elfu moja na mia tano kabla Kristo hajaja!

838 Na wanawake wa wakati wetu watafanya nini? Je, watasema: *“Matarajio hayo ni ya mbali mno kunivutia. Kama ningeona kwamba kwa juhudi kubwa na kujikana sana, jambo lolote la maana lingeweza kufikiwa katika wakati wangu, hilo lingekuwa jambo tofauti. Lakini kidogo ninachoweza kufanya ili kuharakisha uinjilisti wa ulimwengu na kuja kwa Kristo hakitaleta tofauti yoyote. Sina hamu ya kufundisha, kuhubiri au kuomba hadharani. Sitaki kuwa mmoja wa wale wanaotangaza daima kwamba Kristo anarudi, kisha harudi kamwe. Hao ni watu wa kuchekwa. Siwezi kujiunga nao.”* Watu kama hao *“hawahesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri”*.

“Wanawake wa wakati wetu watafanya nini? Je, watasema: ‘Matarajio hayo ni ya mbali mno kunivutia?’ ”

839 Tutakuwa wa kundi lipi? Hilo ndilo swali ambalo kila mmoja wetu wanawake lazima alijibu. Kusitasita hakuna faida katika jambo hili. Ahadi kubwa na unabii mkubwa – mkubwa kuliko yote katika Biblia nzima – viko mbele yetu wanawake. Hakuna njia ya kukwepa; lazima ama tuchague kilicho bora zaidi kinachowezezekana, kikitazamwa kutoka mahali pa juu kabisa, au sivyo tujionyeshe kuwa akina Esau. Mungu ameiweka imani yetu mbele ya changamoto hii. Je, tuidharau haki yetu ya mzaliwa wa kwanza? Mungu apishe mbali!

Kuanzia kitabu cha Mwanzo hadi Ufunuo Katharine C. Bushnell anatoa maelezo ya kina ya (karibu) kila kifungu cha Biblia kinachowahusu wanawake. Kama mtaalamu wa lugha za Kiebrania na Kigiriki, anachunguza vifungu hivyo katika lugha zake za asili na katika muktadha wake wa kihistoria, na kwa njia hiyo anagundua mambo ambayo wakati mwingine yamefichwa na watafsiri wa Biblia. Kitabu hiki kilitokana na juhudi za Bushnell za maisha yake yote za kuleta mageuzi ya kijamii kwa ajili ya wanawake, ambapo aliona uhusiano kati ya hadhi ya wanawake na kutoelewa Maandiko Matakatifu. Watafiti wameitegemea kazi yake ya kufungua njia tangu ilipochapishwa mara ya kwanza mwaka 1921, na wanaiona kuwa mojawapo ya njia bora kabisa zinazotazama Biblia nzima katika swali la nafasi ya mwanamke katika kanisa, katika familia na katika jamii.

Amka, Hawa — kwa maana mbingu ziko karibu kukujia!

Katharine C. Bushnell (1855-1946) alikuwa mtumishi wa Mungu jasiri na mwenye vipawa, aliyeufanya mstari “Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu” kuwa kauli mbiu ya maisha yake. Alikuwa daktari, mmisionari, mwanamageuzi, mwandishi na mzungumzaji, na pia msomi hodari na mbunifu aliyezungumza lugha saba na kujua vizuri Kigiriki cha kale na Kiebrania. Bushnell aliiacha kazi ya udaktari ili kufanya kile alichokiona kuwa kazi muhimu zaidi, yaani kubadilisha hali za maisha zinazowadhalilisha watu, kwa kuchukua nafasi ya uongozi katika Women’s Christian Temperance Union (WCTU) ya vuguvugu la wanawake la karne ya 19. Nafasi ya wanawake kwa mujibu wa Biblia ilikuwa jambo kubwa sana kwa Bushnell, kwa kuwa alifikia hitimisho kwamba tafsiri zenye makosa ndizo zilizosababisha wanawake kutiishwa katika jamii na katika mambo ya kiroho. Mwaka 1896 aliiacha WCTU ili kutumia miaka yake iliyobaki kuandika na kueneza ukweli wa Biblia kuhusu kusudi la asili na lisilobadilika la Mungu la usawa kamili wa wanawake.



Kitabu cha kusoma na kujifunza chenye masomo 100 + nafasi ya kuandika maelezo

ISBN 978-3-94447-225-6 (RVB)

ISBN 978-3-86269-206-4 (VKW)

Tanbihi

1. Kwa sababu ya urefu wa maneno “Agano la Kale” na “Agano Jipya”, katika masomo haya yanayofuata AK inasimama kwa neno la kwanza na AJ kwa la pili, huku herufi kubwa M. ikimwelekeza mwanafunzi kwenye usomaji wa pembeni (ukingoni mwa ukurasa) wa mstari katika yote mawili.
2. Jinsi Hamori alivyomtendea Dina, miongoni mwa Wahivi hao wa zamani, kwa kweli ilimaanisha ndoa. Kwamba Yakobo alikuwa na binti wengine tunajua kutokana na Mwanzo 46:7.
3. *The Herods*, uk. 15
4. Talmud ina nukuu “zisizopungua arobaini” kutoka kwa Ben Sira – *Lange’s Commentaries*, Apokrifa, uk. 276.